JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# USHIRIKI WA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KATIKA KONGAMANO LA TANO LA KIMATAIFA LA UCHUMI WA BULUU



## (BEC 2026)

## KAULI MBIU

**“Mfumo wa kisheria unaotabirika, wenye mizania na rafiki kwa uwekezaji kwaajili ya uchumi endelevu wa Bluu.”**

## JUKUMU LA WIZARA KATIKA KUENDELEZA UCHUMI WA BULUU.

Wizara ya Katiba na Sheria ina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya kisheria yanayohusu utajiri asili na maliasili za nchi. Kwa mujibu wa kifungu cha 3 cha Sheria Sura ya 449 na Sheria Sura ya 450, rasilimali za maji na rasilimali za majini ni sehemu ya utajiri asili na maliasili za nchi. Hivyo, maendeleo ya Uchumi wa Buluu yana uhusiano wa moja kwa moja na jukumu la Wizara katika kusimamia masuala ya kisheria yanayohusu utajiri asili na maliasili.

Sheria Sura ya 449 inaweka msingi wa kulinda mamlaka ya kudumu ya Taifa juu ya utajiri na rasilimali asilia na kuhakikisha matumizi yake yanafanyika kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na wananchi. Katika Uchumi wa Buluu, msingi huu unawezesha uwekezaji unaolinda rasilimali, kuongeza thamani, kukuza uchumi wa ndani na kuhakikisha matumizi yake yanaendelea kuwa na manufaa kwa vizazi vya sasa na vijavyo.



Sheria Sura ya 450 zinaweka mfumo wa kupitia na kushughulikia masharti yasiyo na usawa katika mikataba ya utajiri na rasilimali asilia. Hivyo, sheria hii inasaidia kuhakikisha kuwa mikataba ya uwekezaji inalinda maslahi ya Taifa, huku ikiweka mazingira ya uwekezaji yenye usawa, uwajibikaji na manufaa ya pamoja.



# UCHUMI WA BULUU NA DIRA YA TAIFA YA MAENDELEO 2050

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inalenga kujenga uchumi shindani, jumuishi na endelevu kwa kutumia ipasavyo rasilimali na fursa za Taifa. Katika kufikia azma hiyo, Uchumi wa Buluu una nafasi muhimu katika kuchochea uwekezaji, uzalishaji, ajira na ustawi wa wananchi kupitia matumizi endelevu ya rasilimali za bahari na maji




Sheria Sura ya 449 na 450 zinaunga mkono utekelezaji wa Dira 2050 kwa kuweka msingi wa kisheria unaounganisha ulinzi wa rasilimali, uwekezaji wenye tija na matumizi endelevu. Katika Uchumi wa Buluu, mfumo huu unalenga kuhakikisha kuwa rasilimali zinatumika kuongeza thamani, kuzalisha ajira na mapato, huku manufaa ya uwekezaji yakichangia maendeleo ya Taifa na ustawi wa wananchi.

**Wizara ya Katiba na Sheria,**
**Mji wa Serikali, Mtumba**
S.L.P 315,
40484 DODOMA.

Simu: +255 262 310 019
Piga Bure: 0800 004 004
Nukushi: 255 262 310 056
Barua pepe: km@sheria.go.tz

Katiba na Sheria

www.sheria.go.tz